# Kielelezo cha taarifa kuhusu Watoto Wanaozaliwa Wafu Tanzania



## Nini maana ya mtoto aliyezaliwa mfu?

Mtoto kuzaliwa mfu ni pale ambapo mtoto mwenye uzito unaozidi gramu 1000, ambaye ana wiki zaidi ya 28 toka kutungwa kwa mimba anazaliwa pasipo kuwa na dalili za uhai[1], Sababu kuu za mtoto kuzaliwa mfu ni pamoja na:

- Matatizo wakati wa kujifungua
- Maambukizi pamoja na matatizo yatokanayo na ujauzito (malaria, kaswende, VVU, kisukari, shinikizo la damu)
- Matatizo katika ukuaji wa kijusi (foetus)
- Matatizo ya kimaumbile[2]

Karibu nusu ya vifo vyote vya watoto wanaozaliwa wafu hutokea wakati mama ana uchungu[3], na hivyo kuitwa vifo vya wakati wa kuzaliwa. Vifo vingi vinaweza kuzuilika kwa kuhakikisha huduma bora kutoka kwa wahudumu wenye ujuzi wakati wa kujifungua[1]. Kiwango cha vifo vya watoto wakati mama yuko kwenye uchungu ni kipimo cha ubora wa huduma wakati wa kujifungua, ingawa kuna matatizo katika kutunza kumbukumbu za matokeo ya mimba hasa pale ambapo akinamama hawajifungulii katika vituo vya kutoa huduma za afya[3].

## Watoto kuzaliwa wafu ni tatizo kubwa la kijamii Tanzania.

Takribani watoto 47,000 huzaliwa wamekufa hapa Tanzania, Tanzania ni nchi ya 9 kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa wamekufa duniani[3], karibu nusu ya vifo hivi (22,000) hutokea wakati wa kujifungua, na hivyo kuonyesha uhitaji mkubwa wa uangalizi bora wakati wa kujifungua[3]. Jitihada kubwa zinahitajika ili kulipatia ufumbuzi tatizo hili la watoto kuzaliwa wamekufa, kwa kuwekeza na kuchukua hatua zenye kuleta tija kwa watoto wachanga na akinamama[3].

## Nini kifanyike Tanzania?

Ili kumaliza/kuzuia tatizo la watoto kuzaliwa wafu ni lazima kuwekeza na kuimarisha mfumo wa afya na huduma za uzazi, kuwekeza katika mambo mtambuka ambayo yanawanufaisha akinamama na watoto wachanga pamoja na kuhakikisha kwamba wanakuwepo wahudumu wenye ujuzi na vifaa muhimu ili kusaidia wazazi kila mara. Hatua mahususi za kupunguza watoto kuzaliwa wamekufa ni:

- Kuimarisha huduma za uangalizi wakati wa kujifungua, kuongeza idadi ya akinamama wanaojifungua kwa kusaidiwa na wahudumu wenye ujuzi, na kuhakikisha uwepo wa huduma kamili za uzazi wa dharura
- Kupanua huduma ya kuwasadia watoto kupumua, ili kuwasaidia watoto wanaoshindwa kupumua baada ya kuzaliwa—huduma ambayo imeonyesha kupunguza kifo kimoja katika kila vifo vinne (24%) katika Utafiti wa majaribio Tanzania[4]
- Kuhakikisha kila mama anahudhuria kliniki ya wajawazito mara nne ili kuangalia na kutambua viashiria vya hatari, maambukizi, mambo yasiyo ya kawaida katika ujauzito, na kuwezesha uchungu pale ambapo mimba inapita wiki 41 tangia kutungwa
- Kuzuia malaria[1]

Mwaka 2014 Tanzania iliweka dhamira ya kutekeleza Mpango Kazi wa Kila Mtoto Mchanga[1] na Mpango Mkakati Ulioboreshwa[5]. Mikakati hii inaonyesha vipaumbele ambavyo ni suluhu kwa matatizo haya, inahimiza nguvu za pamoja ili kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya watoto wachanga wanaozaliwa wafu na vifo vya akinamama. Tuipe kipaumbele mikakati yenye kuzingatia ushahidi, hatua rahisi na zenye ufanisi katika vituo vyote vya huduma za afya vinavyotoa huduma za ujauzito na uzazi, pamoja na kuhakikisha kwamba tunakusanya takwimu bora juu ya matokeo ya ujauzito ili kuwezesha kuchukua hatua za haraka pale zinapohitajika.

**Kama mpango mkakati ulioboreshwa utatekelezwa, maisha ya watoto wachanga 9,400 yaweza kuokolewa na kuepusha watoto 2,500 kuzaliwa wafu na kuzuia vifo vya akina mama vipatavyo 1,400 ifikapo Desemba 2015**




## Watoto wanaozaliwa wafu Tanzania

| | |
|---|---|
| **Idadi ya watoto wanaozaliwa wafu (2011)[3]** | **47,000** |
| Idadi ya watoto wanaozaliwa wafu kutokana na matatizo wakati wa kuzaliwa (2011)[3] | 22,000 |
| **Nafasi ya nchi kidunia kwa idadi ya watoto wanaozaliwa wafu (2011)[3]** | **9th** |
| Nafasi ya nchi kidunia kwa idadi ya watoto wanaozaliwa wafu kutokana na matatizo ya wakati wa kujifungua (2011)[3] | 8th |
| **Kiwango cha watoto wanaozaliwa wafu (2011)[3]** | **25.9 kwa vizazi 1000** |
| Kiwango cha watoto wanaozaliwa wafu kutokana na matatizo wakati wa kujifungua (2011)[3] | 12.0 kwa vizazi 1000 |
| **Nafasi ya nchi kidunia kwa kiwango cha watoto wanaozaliwa wafu (2011)[3]** | **21st** |
| **Nafasi ya nchi kidunia kwa kiwango cha watoto wanaozaliwa wafu kutokana na matatizo ya wakati wa kujifungua (2011)[3]** | **24th** |
| Mahudhurio kliniki mara nne au zaidi(2010)[6] | 43% |
| **Kiwango cha akinamama wajawazito wanaokunywa dawa za kuzuia malaria wakati wa mahudhurio ya kliniki [6]** | **68%** |
| Kiwango cha kuhudumiwa na mhudumu mwenye ujuzi wakati wa kujifungua(2010)[6] | 49% |
| **Vituo kutoa huduma za afya ya msingi vinavyotoa huduma za dharura za uzazi (BEmONC)[7]** | **39%** |
| Hospitali zinazotoa huduma za dharura za uzazi (CEmONC)[7] | 73% |

## Marejeo:


1. World Health Organization, & UNICEF. (2014). Every Newborn: An Action Plan to End Preventable Deaths. Geneva: WHO.
2. World Health Organization. Maternal, newborn, child and adolescent health: Stillbirths. Retrieved 31 October 2014 from www.who.int/maternal_child_adolescent/epidemiology/stillbirth/en/
3. Lawn, J.E., Blencowe, H., Pattinson, R., Cousens, S., Kumar, R., Ibiebele, I., Gardosi, J., Day, L.T., & Stanton, C. (2011). Stillbirths: Where? When? Why? How to make the data count? *The Lancet, 377*(9775), 1448-63.
4. Msemo, G. (2014). Implementation of the HBB program in Tanzania - Comprehensive final report. Available at www.helpingbabiesbreathe.org/reports.html
5. Ministry of Health and Social Welfare [United Republic of Tanzania]. (2014). *The National Road Map Strategic Plan to Accelerate Reduction of Maternal Newborn and Child Deaths in Tanzania 2008-2015. Sharpened One Plan April 2014*. Dar Es Salaam: MoHSW.
6. National Bureau of Statistics [Tanzania], & ICF Macro. (2010). *Tanzania Demographic and Health Survey 2010*. Dar Es Salaam/Calverton: NBS, ICF Macro.
7. Ministry of Health and Social Welfare [United Republic of Tanzania]. (2013), *Mid Term Analytical Review of the Performance of the Health Sector Strategic Plan III (2009-2015). September 2013*.


**Novemba 2014**